**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI ANUAI NA. 208 YA 2022**

**BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA**

**ELIMU YA JUU ...............................................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**YUSUFU M. KISALE ....................................... MJIBU MAOMBI**

**MAAMUZI MADOGO**

**15.08 & 02.09.2022**

**Rwizile, J**

**BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU** imeleta maombi haya Mahakamani ikiomba kuwekwa kando kwa amri ya kuyafuta maombi Na. 104 ya 2022 yaliyotolewa na Mahakama haya (Mhe. Jaji Rwizile) ya tarehe 25.04.2022.

Ilielezwa kuwa mleta maombi aliwasilisha maombi yaliyopewa Na. 401 ya 2021 ya kuongezewa muda ili aweze kuwasilisha taarifa ya kusudio la kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani dhidi ya Mahakama hii.

Tarehe ya shauri ya kusikilizwa ilikuwa ni 25.04.2022 saa nne asubuhi. Muda ulifika, na wakili wa Serikali alichelewa kufika Mahakamani kwa

dakika 10 na kufahamishwa na wakili wa upande wa pili na baadae karani kuwa maombi hayo yameondolewa kwa kutokuhudhuria kwake.

Mleta maombi ameeleza kuwa sababu ya kuchelewa kufika Mahakamani ni kutokana na kupatwa na maradhi ya tumbo lililokuwa likimsokota na kumsababishia maumivu makali. Hali hiyo ilimsababishia kupitia katika kituo cha afya ili kufanyiwa vipimo.

Maombi haya yameletwa Mahakamani hapa yakiambatanishwa na kiapo cha wakili wa Serikali kwa niaba ya mleta maombi ambacho kilipingwa na kiapo kinzani cha mjibu maombi.

Sababu ya maombi haya ya kisheria ni *endapo zipo sababu za msingi za kutoa amri ya kuondoa/kuweka kando amri ya kufuta ombi namba 401 la 2022 na kurudisha ombi hilo ili lisikilizwe kwa kina.*

Kila upande ulipata wasaha wa kuwakilishwa. Mleta maombi aliwakilishwa na wakili wa Serikali, Bwana Elias Evelius Mwendwa wakati mjibu maombi aliwasilishwa na Bi. Blandina Kihamba, Wakili Msomi.

Bwana Elias aliwasilisha kama ifuatavyo, shauri lilipangwa tarehe 25.04.2022 kwa ajili ya kusikilizwa. Siku hiyo mleta maombi alifika kwa kuchelewa Mahakamani kwa dakika 10 kwakuwa alipatwa na ugonjwa wa tumbo na alikuwa na maumivu makali. Hali hiyo ilimfanya aende katika

kituo cha afya na kufanyiwa vipimo. Alithibitisha maelezo yake kwa kuambatanisha kielelezo OSG1.

Alieleza kuwa mleta maombi hakufika kwa wakati siku hiyo kutokana na ugonjwa na hivyo ameiomba Mahakama kulirudisha shauri ilikusikilizwa kwakuwa mjibu maombi hatopata dhala lolote.

Katika kujibu hoja, Bi. Blandina aliwasilisha kuwa maombi ya mleta maombi hayana mashiko kwakuwa sabau zimetolewa baada ya shauri kufutwa. Alifafanua zaidi kwa kueleza kuwa wakili wa Serikali wa mleta maombi siku ya shauri kusikilizwa alichelewa bila ya sababu ya msingi kama alivyoeleza katika aya ya 3 ya kiapo chake kinzani.

Bi Blandina aliwasilisha kuwa ushahidi wa OSG1 uliotolewa na wakili wa mleta maombi hauna vigezo kwasababu kwenye nyaraka hakuna ugonjwa uliotajwa, haina tarehe aliyofika katika kituo cha afya na pia nyaraka inaeleza asifanye kazi lakini walimwona Mahakamani.

Aliwasilisha tena kuwa mleta maombi aliichezea haki yake mwenyewe tayari na ndio maana alikuwa ameleta maombi ya kukata rufaa nje ya muda. Akaeleza kuwa mleta maombi amekuwa mzembe katika kutafuta haki zake na hivyo anachelewesha muda ana utekelezaji pia. Akamalizia kwa kuomba maombi ya mleta maombi yaweze kutupiliwa mbali.

Baada ya kupitia mawasilisho ya pande zote mbili, Mahakama hii imekuwa na hoja moja ya kujadili ya *endapo mleta maombi ameweza kuithibitishia Mahakama kuwa alikuwa na sababu za msingi kuchelewa mahakamani.*

Katika shauri hili, kanuni ya 36(1) na kanuni ya 38(1)(a)(c) and (2) vyote toka katika Kanuni za Mahakama ya Kazi, TLS 106 ya 2007 ambavyo vinaelekeza shauri linaweza kurejeshwa Mahakamani baada ya mleta maombi kuonyesha sababu za msingi zilizompeleka kutokufika Mahakamani katika tarehe ya kusikilizwa.

Mleta maombi alieleza kuwa alichelewa kufika Mahakamani siku husika ya kusikiliza maombi yake kwakua alisumbuliwa na tumbo hali iliyompelekea kufika hospitali.

Mjibu maombi alipinga vikali hoja hiyo kwa kueleza kuwa sababu ya mleta maombi haina mashiko kwani walikutana Mahakamani siku hiyo na alikuwa vizuri. Pia kwa kieleleza alichokifikisha Mahakamani kilikuwa hakina tarehe, ilimpa pumziko wakili huyo wa Serikali la siku nzima lakini bado alifika Mahakamani.

Mahakama katika kupitia kielelezo kilichofikishwa Mahakamani OSG1 kinaeleza kuwa Elias Evelius Mwendwa kuruhusiwa kutokufanya kazi kwa siku hiyo moja. Lakini katika kuendelea mbele zaidi imebaini nyaraka ya taarifa ya uwakilishi ambayo inaeleza wazi kuwa mleta maombi

atawakilishwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Kwa urahisi wa rejea:

-

"***NOTISI YA UWAKILISHI***

...

*KWAMBA, Mleta Maombi anaitaarifu Mahakama Kuu divisheni ya Kazi Pamoja na Mjibu Maombi kuwa katika maombi haya atawakilishwa na* ***OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI.***"

Kwa mantiki hiyo mleta maombi anawakilishwa na ofisi na sio mtu mmoja. Hivyo ofisi ilistahili kumfikishwa wakili mwingine wa Serikali kuweza kuendelea na kusikiliza maombi hayo kwakuwa Elias Evelius Mwendwa sio ofisi bali ni mmoja wa watumishi katika ofisi hiyo.

Mahakama haya baada ya kupitia maombi haya inaona kwamba maombi yaliyowasilisha kutokuwa na mashiko kwa kukosa sababu za msingi. Na hivyo yametupiliwa mbali. Na kwakuwa hili ni shauri la mgogoro wa kikazi, kila upande utajilipia ghalama zake.

**A.K. RWIZILE**

**JAJI**

**02.09.2022**